MUHAS SACCOS LTD

Contact: muhassaccosltd@gmail.com Phone: +255786213138

Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili

UTANGULIZI

Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kilianzishwa mwaka 2006 na kuandikishwa rasmi mwaka 2008 na kupata hati ya usajili namba DRS 1049.

TASWIRA

Kuwa asasi bora ya ushirika wa akiba na mikopo yenye kutoa bidhaa na huduma madhubuti za fedha zinazohitajika na kutumiwa na wanachama wake kwa kuwashirikisha wanachama na watendaji wenye ujuzi na uwezo wa kuendesha Saccos ya kisasa kibiashara.

SIFA ZA KUWA MWANACHAMA

- Awe mwenye umri usiopungua miaka 18.
- Awe na tabia nzuri na akili timamu.
- Awe amelipa kiingilio na hisa, na awe anaweka akiba.
- Awe mwaminifu na mwadilifu.
- Awe tayari kufuata masharti ya chama.
- Awe raia wa Tanzania kwa kuzaliwa au kuandikishwa na anayekubalika kwenye masharti ya MUHAS SACCOS.

- Awe mfanyakazi au mwanachama mstaafu wa chuo kikuu cha Afya na sayansi shirikishi Muhimbili (MUHAS), Hospitali ya taifa Muhimbili, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) na Taasisi ya mifupa (MOI).

FAIDA ZA CHAMA

- Kukuza utamaduni wa kujiwekea akiba leo hii na kusaidia familia yako baadae.
- Kushiriki katika masoko ya mitaji na kupata faida.
- Kupata mikopo yenye masharti nufuu.
- Kushiriki kikamilifu katika kutekeleza mpango wa MKUKUTA (Mpango wa kukuza uchumi na kuondo umasikini).
- Kupata ushauri juu ya matumizi na uwekezaji bora wa mikopo wanayochukua
- Kutatua changamoto mbalimbali za kifedha kwa wanacham.

HUDUMA ZITOLEWAZO NA CHAMA

- Kutunza akiba, amana pamoja na kumbukumbu za kifedha za wanachama wake.
- Kutoa mikopo yenye masharti na riba nafuu kwa wanachama wake.
- Kuendesha semina na mikutano mbalimbali kwa wanachama wake.

AINA ZA MIKOPO ITOLEWAYO

- Mikopo ya maendeleo
- Mikopo ya dharura
- Mkopo wa anza maisha
- Mikopo ya sikukuu

UTARATIBU WA UTOAJI WA MIKOPO

- Mwombaji wa mkopo atahitajika kujaza fomu maalum ya maombi ya mkopo husika akitaja jina lake kamili, kiasi anachoomba, dhamana zake pamoja na wadhamini wawili ambao ni wanachama wa MUHAS SACCOS LTD.
- Fomu iambatanishwe na current salary slip, pamoja na kitabu cha uanachama
- Mwombaji lazima awe amelipa kiingilio, amechangia akiba kwa muda usiopungua miezi mitatu na kumiliki angalau hisa tano kati ya kumi zinazohitajika.
- Mwanachama ataruhusiwa kukopa kiasi kisichozidi mara tatu ya akiba yake.

UTARATIBU WA MALIPO

Kwa wafanyakazi, makato hufanywa moja kwa moja kupitia mishahara (payroll system). Na kwa wanachama wasio wafanyakazi, na wastaafu hurejesha kwenye benki kupitia akaunti ya MUHAS SACCOS LTD kwa namba 20901600013 NMB tawi la Muhimbili kulingana na tarehe walizopangiwa.

HAKI ZA MWANACHAMA

- Kushirika katika shughuli zote za MUHAS SACCOS kwa kufuata masharti ya MUHAS SACCOS na maazimio yote ya Mikutano mikuu.
- Kuhudhuria na kutoa maoni yako katika mikutano yote ya MUHAS SACCOS kwa mujibu wa sheria
- Kuweka na kutoa akiba, amana na hisa zako kwa kufuata kanuni za MUHAS SACCOS
- Kuchagua au kuchaguliwa kuwa kiongozi
- Kutazama mizania, mihutasari ya mikutano.

WAJIBU WA MWANACHAMA

- Kulipa kiingilio, kununua hisa na kuweka akiba kwa mujibu wa masharti ya MUHAS SACCOS, pamoja na kukopa kwa busara.
- Kuwa mwaminifu kwa MUHAS SACCOS na kushiriki kikamilifu katika shughuli za chama ili kukamilisha malengo yake.
- Kuhudhuria mikutano yote ya wanachama na kupewa taarifa za maendeleo ya chama.
- Kulipa mkopo kwa muda uliopangwa kulingana na masharti
- Kutunza kitabu chake cha uanachama.

MALENGO YA CHAMA

- Kuongeza wanachama kwa kuhakikisha kuwa zaidi ya nusu ya wafanyakazi wa MUHAS wanakuwa wanachama wa MUHAS SACCOS LTD.
- Kuboresha mfumo wa utendaji kuwa wa kisasa wenye mtandao wa technolojia mpya.
- Kuongeza bidhaa mbalimbali za kifedha mfano, mkopo wa elimu sikukuu ujenzi, fao la kustaafu n.k.
- Kufungua tawi kwenye kampasi ya mloganzila ili wateja wetu wapate huduma kwa ukaribu
- Uwekezaji kwa njia ya kununua hisa za makampuni mbalimbali kwa lengo la kuongeza faida ya chama.
- Kuendelea kutoa semina mbalimbali kwa wanachama wetu kwa lengo la kuwasaidia kutumia vizuri mikopo tunayo wakopesha kwa ajili ya kuwasaidia kuanzisha miradi.

JINSI YA KUJIUNGA NA CHAMA

- Mwombaji anatakiwa kujaza fomu ya maombi ya kujiunga na chama inayotolewa kwenye ofisi ya chama.
- Mwombaji atatakiwa kulipa kiingilio cha shilingi elfu kumi na tano (15,000/=) tu.
- Mwombaji atatakiwa kumiliki angalau hisa zisizopungua tano (5) kati ya kumi zinazohitajika. Zenye thamani ya shilingi elfu thelathini (30,000/=) kwa kila hisa moja ndani ya miezi mitatu baada ya kujiunga.
- Mwombaji atatakiwa kujiwekea akiba kwa kiasi kisichopungua elfu hamsini (50,000/=) kwa kila mwezi.

MAHALI OFISI ILIPO

Makao makuu ya chama yako ndani ya Chuo Kikuu cha afya na sayansi shirikishi Muhimbili, katika jengo la Estate Block “K”